TANGAZO LA SERIKALI NA. 251A la tarehe 2/9/2026

SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, (SURA 343)

NOTISI

(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 49(2))

NOTISI YA KUWEPO KWA NAFASI WAZI YA KITI CHA UBUNGE
KATIKA JIMBO LA CHAMWINO YA MWAKA 2026

SURA 343 KWA KUWA, Kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, kinampa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka ya kutangaza nafasi wazi ya Ubunge pale Mbunge anapojiuzulu, anapofariki au anapoacha nafasi ya Ubunge kwa sababu nyingine tofauti na zilizoainishwa chini ya kifungu cha 142 cha Sheria hiyo;

SURA 2 NA KWA KUWA, tarehe 26 Agosti 2026, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mamlaka aliyopewa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, alimteua Mhe. DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chamwino kwa udhamini wa Chama cha Mapinduzi (CCM), kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na uteuzi huo ulithibitishwa na Bunge tarehe 28 Agosti, 2026;

SURA 2 NA KWA KUWA, Ibara ya 71(1)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inaeleza kuwa Mbunuge atakoma kuwa Mbunge na ataacha kiti chake katika Bunge iwapo atachaguliwa au atateuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivyo kutokana na uteuzi huo wa Mhe. DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI amekoma kuwa Mbunge na Kiti chake kiko wazi.

GN. No. 251A (Contd)

SURA 343

KWA HIYO SASA, Mimi MUSSA AZZAN ZUNGU, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 49(2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, ninautaarifu umma kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kuwepo kwa Nafasi Wazi ya Kiti cha Ubunge katika Jimbo la Chamwino ya Mwaka 2026.

Tangazo

2. Kiti cha Ubunge wa Jimbo la Chamwino kinatangazwa kuwa kipo wazi.

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

Dodoma,
1 Septemba, 2026

MUSSA AZZAN ZUNGU
Spika